

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS,**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

Telephone:0262968010  
Fax:0262968010  
Website:www.kilolodc.go.tz  
Email:ded@kilolodc.go.tz/ ded.kilolo@iringa.go.tz

S.L.P2324,  
KILOLO .  
Tanzania



Kumb. Na. KDC/AB/41/22

24/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA KUKUSANYA**  
**TAARIFA ZA ANWANI ZA MAKAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiloilo anakaribisha maombi ya Watanzania wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya kukusanya taarifa na kuingiza kwenye mfumo wa Anwani za Makazi.

**1.0 OFISA USAJILI ANWANI ZA MAKAZI MSAIDIZI**

**2.0 SIFA ZA MWOMBAJI**

Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya cheti cha Kompyuta katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**A. KAZI NA MAJUKUMU YA OFISA USAJILI ANWANI ZA MAKAZI MSAIDIZI**

- I. Kubandika vibao vyenye majina ya mitaa/kijiji vilivyopitishwa na kamati ya wataalaamu wa Anwani za Makazi.
- II. Kuainisha namba za nyumba
- III. Kusajili taarifa mbalimbali za huduma kwenye mfumo wa Anwani za Makazi.
- IV. Kusajili taarifa za Anwani tegemezi kwenye makazi
- V. Kusajili taarifa za Mmiliki wa Anwani
- VI. Kusajili taarifa za Wategemezi wa mmiliki wa Anwani
- VII. Kukusanya na kuingiza taarifa kwenye mfumo wa Anwani za Makazi.
- VIII. Usajili wa taarifa za Anwani (Anwani Kuu)

**B. MASHARTI YA KAZI/WAOMBAJI KWA UJUMLA**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 35.
- ii. Awe na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu janja (smartphone) inayoendeshwa na mfumo wa android yenye uwezo wa uhifadhi wa GB 32 au zaidi (freespace GB 32 au zaidi) yenye uwezo wa kuhifadhi chaji masaa 12 au zaidi.
- iv. Awe na barua pepe hai (email).
- v. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa muda mrefu.
- vi. Awe na uelewa unaokidhi wa jiografia ya Kijiji au Mtaa husika.
- vii. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, cheti cha kuzaliwa na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- viii. Picha Mbili "Passport Size" zilizopigwa siku za karibuni na hakikisha imeandikwa jina lako kwa nyuma. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahusika/mhusika kuchukuliwa hatua za kisheria.
- ix. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na yapitishwe kwa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anapotokea mwombaji.
- x. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **03/03/2022 saa 9:30 alasiri.**

Aidha, barua za maombi zinaweza kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
S.L.P 2324,  
**KILOLO**

**Limetolewa na:**

  
LAIN E. KAMENDU  
MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
**KILOLO**  
MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KII OI O